

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA  
Simu Na: (026) 2322848, 2321607,  
2322853, 2322420,  
Nukushi: (026) 2322116, 2322146.  
2321013,  
Barua pepe:[ps@tamisemi.go.tz](mailto:ps@tamisemi.go.tz)

Unapojibu tafadhali taja:-



Tawala za Mikoa na  
Serikali za Mitaa,  
S. L. P. 1923,  
DODOMA.

Kumb. Na. EB.151/297/02/'N'/127

31 Januari, 2017

Makatibu Tawala wa Mikoa,  
**TANZANIA BARA**

**Yah: MAFUNZO YA UTUMIAJI NA UENDESHAJI WA TOVUTI ZA MIKOA NA  
MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA WATAALAM WA TEHAMA NA  
HABARI**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Sekta ya Umma (PS3) inaendelea zoezi la kuboresha mifumo ya TEHAMA inayotumika katika taasisi zake ikiwa ni pamoja na kuhuisha/kutengeneza upya Mfumo wa Tovuti (*Government Website Framework-GWF*) kwa ajili ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopo ndani ya Mradi wa PS3.

Kazi ya kutengeneza Mfumo wa Tovuti (GWF) ilifanywa na timu ya wataalam wa TEHAMA kutoka OR-TAMISEMI, Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) na watalaam kutoka Mikoa na Halmashauri. Lengo kuu la kuwatumia watalaam wa Serikali ni kuwajengea uwezo wa kumiliki mifumo na kuiendeleza.

Hatua iliyofikiwa ni kutoa mafunzo kwa watalaam wa TEHAMA na Habari katika ngazi ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa juu ya utumiaji na uendeshaji wa Tovuti. Mafunzo yatatolewa kwa watalaam wote wa Mikoa na Halmashauri nchini kwa kuzingatia kuwa, Mfumo wa Tovuti (GWF) uliotengenezwa unaweza kutumika na Taasisi yoyote ya Serikali kulingana na mahitaji husika.

Aidha, kwa watalaam wanaotoka Mikoa na Halmashauri (wawili kwa kila Mkoa na Halmashauri) ambayo ipo chini ya Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Sekta ya Umma (PS3), gharama za usafiri wa Umma na posho za kujikimu zitalipwa na Mradi wa PS3.

Kwa barua hii, unaombwa uzielekeze Halmashauri zilizopo chini ya Mkoa wako ili kijiandaa kuwagharamia watalaam wawili, Afisa TEHAMA na Habari kutoka ngazi ya Mkoa na Halmashauri (Hii ni kwa ile Mikoa na Halmashauri nje ya mradi wa PS3 tu) kushiriki mafunzo haya muhimu kwa vitendo. Sambamba na hilo, washiriki wote wajulishwe kuja na kompyuta mpakato (laptop) pamoja na taarifa ambazo zitaingizwa katika tovuti ya Mkoa na Halmashauri yake ili kipindi watakapomaliza mafunzo tovuti ziwe tayari kwa matumizi na taarifa sahihi. Ili kujua vipengele vya kuwekewa taarifa katika tovuti zenu tafadhali (*Angalia Kiambatisho Na 2*) au tembelea [egatest.go.tz/gwf](http://egatest.go.tz/gwf).

Mafunzo yatafanyika kwa awamu mbili, kuanzia tarehe 13/02/2017 hadi tarehe 20/02/2017 kwa Mikoa ya **Kagera, Mwanza, Mara, Simiyu na Shinyanga** na baadae kufanyika nchi nzima kwa kanda mbalimbali kuanzia tarehe 13/03/2017 hadi 23/03/2017 (*Angalia Kiambatisho1*).

Nakutakia utekelezaji mwema.



Eng. Mussa Iyombe  
**KATIBU MKUU**

Nakala:      Mkurugenzi wa Mradi wa PS3,  
                  S.L.P.32444,  
                  DAR ES SALAAM.

Mtendaji Mkuu,  
Wakala ya Serikali Mtandao,  
S.L.P.4273,  
DAR ES SALAAM.

***Kiambatisho Na 1***

## Kiambatisho Na 1

### ZONES

Region	# LGAs	# Participants	Venue	Zone	Start Date	End Date
Mwanza	8	76	Mwanza	Zone I	13 <sup>th</sup> Feb. 2017	20 <sup>th</sup> Feb. 2017
Kagera	8					
Mara	9					
Simiyu	6					
Shinyanga	6					
Dodoma	8	54	Dodoma	Zone II	13 <sup>th</sup> March 2017	23 <sup>rd</sup> March 2017
Singida	7					
	6					
Iringa	5					
Tabora	8	56	Shinyanga	Zone III	13 <sup>th</sup> March 2017	23 <sup>rd</sup> March 2017
Geita	6					
Kigoma	8					
Katavi	5					
Rukwa	4	46	Mbeya	Zone IV	13 <sup>th</sup> March 2017	23 <sup>rd</sup> March 2017
Njombe	6					
Mbeya	7					
Songwe	5					
Lindi	6	46	Mtwara	Zone V	13 <sup>th</sup> March 2017	23 <sup>rd</sup> March 2017
Mtwara	9					
Ruvuma	7					
Dar es Salaam	6	50	Morogoro	Zone VI	13 <sup>th</sup> March 2017	23 <sup>rd</sup> March 2017
Pwani	9					
Morogoro	9					
Arusha	7	55	Morogoro	Zone VII	13 <sup>th</sup> March 2017	23 <sup>rd</sup> March 2017
Kilimanjaro	7					
Manyara	7					
Tanga	11					

# Kiambatisho Na.2

## 2.1 SITE MAP FOR REGIONAL SECRETARIAT

HOME

ABOUT US

DISTRICTS

- Home
- About Us
  - Mission and Vision
  - History
  - Structure
- Districts
  - Babati
  - Mbulu
  - Hanang
  - Kiteto
  - Simanjiro
  - Ilala
- Departments
  - Human Resources
  - Planning and Management
  - Finance and Accounts
  - Internal Audit
  - Procurement and Supply
  - Economy and Production
  - Infrastructure
  - Local Government
  - Social Welfare
  - ICT
  - Health
  - Education
  - Water

- Publications
  - Forms
  - Guidelines
  - Procedures
  - Reports
- Investments
  - Investment One
  - Investment Two
  - Investment Three
  - Investment Four
  - Investment Five
- Media Center
  - News
  - Announcements
  - Gallery
  - Sports and Games
  - Speeches
  - Press Releases
  - Videos

## 2.2. SITE MAP FOR LOCAL GOVERNMENT AUTHORITIES

Home

About Us

Test M

- Home
- About Us
  - History
  - Mission and Vision
  - Who we Are
- Test Menu
- Administration
  - Organization Structure
  - Units
    - Unit Name
    - Unit Name
    - Unit Name
    - Unit Name
- Publications
  - Guidelines
  - Forms
  - Procedures
  - Reports
  - Acts
- Media Center
  - Press Release
  - Videos
  - Speeches
  - Photo Gallery
- Media Center
  - Press Release
  - Videos
  - Speeches
  - Photo Gallery
  - News
  - Events
- Mission and Vission

### 2.3. TAARIFA ZINAZOTAKIWA WAKATI WA MAFUNZO YA GWF

Na.	AINA YA TAARIFA ZINAZOTAKIWA
1.	Tambua color code ya taasisi (corporate colour) yako na uiandike sehemu
2.	Related links- majina ya tovuti mnazofanya nazo kazi kwa ukaribu eg TAMISEMI, Tovuti Kuu ya Serikali
3.	Contact details za Taasisi
4.	Logo sahihi na yenye ubora ya Halmashauri (Coloured)
5.	Picha za maeneo muhimu ya Halmashauri na Mikoa ambayo kila mtu anaweza kutambua kuwa niko Mafinga au Mwanza hata akiona picha
6.	Administration- organisation structure ikiwa katika <i>image form</i>
7.	<i>Publications</i> kama vile <i>report wazi za mwaka, newsletters, brochures etc soft copy or image</i>
8.	Media Centre, eg picha za matukio yaliyopita na ya sasa, video mbalimbali ambazo mumewahi kurekodi kwa ajili ya umma.
9.	Taarifa ya huduma mbalimbali mnazotoa na jinsi zinavyopatikana.
10.	Fomu mbalimbali anazopewa mwananchi kujaza anapotaka huduma. Fomu hii iwe ambayo <i>si moja ya vyanzo vya mapato kwa halmashauri au mkoa.</i>
11.	Picha za maeneo ya uwekezaji yaliyopo katika mkoa au halmashauri yako.
12.	Matangazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ya zabuni kama yapo.
13.	Picha ya Mkuu wa Mkoa, Wilaya M/Kiti wa halmashauri au Mkurugenzi au RAS (Passport size)
14.	Sheria ndogo zinazotumika katika halmashauri (Bylaws)